

## **TUME YA KIKRISTO YA HUDUMA ZA JAMII**

### **MTIHANI WA PAMOJA WA SHULE ZA MAKANISA KANDA YA KASKAZINI**



### **MTIHANI WA UTAMIRIFU KIDATO CHA SITA 2023**

**121/1**

### **KISWAHILI 1**

#### **MWONGOZO WA USAHIHISHAJI**

1. Mtahini ajibu kama ifuatavyo

- (i) HAKI YA KUPIGA KURA (02)
- (ii) **Huria-** uhuru wa kufanya jambo (0.5)

**Wenye bidii ya kutia-** wasio kata tamaa/ wachapakazi (0.5)

**Viongozi domo kaya-** wazembe/wasiotekeleza majukumu yao (0.5)

**Ujamaa siyo sawia-**wasio penda maendeleo (0.5)

**Kayaya-**wasiotufaa (0.5)

iii) -Husaidia kupata kiongozi bora (01)

-Husaidia kila raia kujuu haki zake za msingi (01)

iv) kuchagua viongozi bora na sio bora viongozi (01)

v)- haki ya kila raia (0.5)

-kuchagua viongozi bora (0.5)

-athari za kutokupatikana kwa viongozi bora (0.5)

-umuhimu wa kila mtanzania kujuu (0.5)

-kupiga kura ni haki ya msingi (0.5)

2. Mtahiniwa atoe tofauti iliyopo kati ya kiwakilishi na kivumishi kwa mifano;

- (i) Tofauti katika maana
- (ii) Tofauti katika aina

- (iii) Tofauti katika mahali pa utokeaji mf. Kiwakilishi hutokea mwanzoni mwa sentensi yaani upande wa kiima wakati kivumishi huweza kutokea upande wa kiima na kiarifu
- (iv) Kiwakilishi husimama badala ya nomino lakini kivumishi akisimami badala ya nomino
- (v) Kivumishi huzungumzia Zaidi kuhusu nomino au kiwakilishi lakini kiwakilishi hakina sifa hiyo (Alama 02) na hoja nyinginezo
3. Mtahiniwa atoe maana ya fasili ya maneno yafuatayo kwa mifano;
- i) Irabu ni sauti ambazo hutamkwa pasipo kuwepo na kizuizi chochote hewa kutoka kwenye mapafu kwenda nje kupitia chembe za kinywa. Mf. /a/, /e/, /i/, /o/ na /u/
  - ii) Unyambulishaji ni uongezaji wa viambishi mwishoni mwa mzizi wa neno. Mf. Piga- pigisha, pigiwa, pigwa
  - iii) Fonimu ni kipashio kidogo cha kifonolojia chenye uwezo wa kubadili maana ya neno. Mf. Pata- kata
  - iv) Kishazi tegemezi ni aina ya kishazi ambacho hakiweza kusimama peke yake na kutoa maana kamili pasipo kutegemea kisgazi huru.  
Mf. Mwalimu aliyejukana jana
  - v) Upatanisho wa kisarufi ni uhusiano uliopo baana ya nomino na viambishi awali za vitenzi katika tungo. Mf. Mtoto anacheza (Alama 02 kila hoja jumla, 10)

4. Mambo ya kuzingatia/yanayomuongoza mtumiaji wa lugha katika utenzi wa rejestani;

- (i) Muktadha
- (ii) Uhusiano baina ya wahusika
- (iii) Mada ya mazungumzo
- (iv) Lengo la mazungumzo
- (v) Jinsi/namna ya mazungumzo ( @ 02 jumla alama 10)

5. Mtahiniwa aandike tangazo kama ifuatavyo:-

- (i) **Jina la mtoa tangazo.**  
**Mfano:** **SHIRIKA LA NGEGE TANZANIA**  
**TANESCO BODI YA UTALII TANZANIA** (Alama 04).
- (ii) **Kichwa cha Tangazo**  
Huandikwa kwa ufupi.

Mfano:- TATIZO LA USAFIRI WA NDEGE  
(Alama 04)

**(iii) Lengo la Tangazo.**

Taarifa zote za msingi za tangazo hutolewa kwa ufupi. Taarifa hizi hutolewa na kile kinachotangazwa. (Alama 08)

**(iv) Cheo/Wadhifa**

***Mfano:***

- Afisa Habari wa shirika la ndege (Alama 04)

**Mtahiniwa aandike Tangazo kama ifuatayo:-**

**SHIRIKA LA NDEGE TANZANIA**

**TANGAZO LA TATIZO LA USAFIRI WA NDEGE**

Tunawatangazia abira wetu kuwa, ndege ya Precision aina ya ATC haitafanya safari yake siku ya tarehe 11/11/2023 saa 1:00 asubuhi na badala yake itafanya safari tarehe 13/11/2023 saa saba mchana.

Mabadiliko hayo yametokana na hali ya ndege ilianguka Novemba 09 katika Ziwa Victoria kutokana na machafuko ya hali ya hewa katika uwanja wa ndege wa Bukoba ila tunaomba radhi watu wote kwa usumbufu uliojitokeza ambao kusema kweli upo nje ya uwezo wetu.

*Venance Kurambate*

*Afisa habari shirika ndege Tanzania.*

6. Mtahiniwa anatakiwa kueleza maana ya lahaja na usanifishaji na namna Kiswahili sanifu kilivyodumaza lahaja nyingine;

Namna Kiswahili sanifu kilivyodumaza lahaja nyingine;

- Kiswahili kutumika katika vyombo vya habari
- Kiswahili kutumika kama lugha ya taifa
- Kiswahili kutumika kutolea elimu
- Kiswahili kutumika katika shughuli za kisiasa

- Kiswahili kutumika katika biashara
- Kiswahili kutumika katika shughuli za kidini  
HOJA 06@3  
UTANGULIZI 01  
HITIMISHO 01

7. Mwanafunzi atoe maana ya kukua kwa kiswahili nchini Kenya - Hoja hizo ni:

- Utangulizi (01 Alama)

Kiini (18 Alama)

- (i) Uwepo wa makabila shupavu nchini Kenya
- (ii) Uwepo wa mbuga za Wanyama
- (iii) Sera mbovu za utawala wa kikoloni
- (iv) Lugha ya kiswahili kupigwa marufuku nchini Kenya
- (v) Lugha ya kiswahili kutumiwa na jeshi la K.A.R
- (vi) Kiswahili kuchukuliwa kama lugha ya kislamu

- Hitimisho (01 Alama)

8. Mtahiniwa anatakiwa kueleza maana ya nadharia kisha aoneshe au aeleze nadharia hizo kutokana na wataalamu hao.

**Nadharia hizo ni kama zifuatazo;**

- i. Nadharia ya usawe wa kimuundo
- ii. Nadharia ya usawe wa kidhima
- iii. Nadharia ya usawe wa aina-matini
- iv. Nadharia changamani.

Hoja 4 @ 04

Utangulizi 02

Hitimisho 02

Jumla alama 20